

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA

29 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA TAREHE 29 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

467. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la OPD katika Kituo cha Afya cha Kata ya Kiloleli Wilayani Busega.

468. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda katika Jimbo la Mwibara.

469. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Maweni - Ng'hoboko – Meatu.

**470. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO
(BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Guta – Bunda Mjini.

WIZARA YA UJENZI:

**471. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI
(UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa vibanda vya abiria katika Vivuko vya Bwisya, Bugorola na Kisorya utaanza kwani fedha ilitengwa Bajeti ya Mwaka 2023/2024.

**472. MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN
AIDAN MWALUKO KABUDI (KILOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja katika Mji wa Kilosa kuvuka Mto Mkondoa ambalo limebomolewa na mafuriko.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA
YA HABARI:**

**473. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini tatizo la mawasiliano ya simu katika baadhi
ya Kata za Jimbo la Mtwara Mjini litaisha.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**474. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI
ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi
na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango maalum wa
kuinua elimu kwenye Mikoa iliyo nyuma kielimu.

WIZARA YA MAJI:

**475. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR
(NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha Vituo vya Afya kwenye mtandao wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria Wilayani Nyang'hwale.

476. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa maji wa Ndaje unaopeleka maji katika Vijiji vya Mbesa *Airport* na Lijimbo utakamilika.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

477. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Askari Wanyama Pori katika Vijiji vya Olchorapus, Imbibia na Engalaoni - Arumeru.

WIZARA YA KILIMO:

478. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Soko la Remagwe - Sirari litajengwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UJENZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

DODOMA
29 MEI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE